OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

SHULE YA SEKONDARI SENG'WA,
S.L.P 367,
MASWA – SIMIYU.
Tarehe ....

Kumb.Na. SESS/J/VOL.1/09

Jina la Mwanafunzi ....

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE.

1. Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule ya sekondari Seng'wa katika kidato cha kwanza mwaka 2020 ni mategemeo yangu kuwa utaitumia nafasi hii vizuri katika kuendeleza kipaji chako kwa muda wote utakaokuwa hapa shuleni.
   Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2020 siku ya Jumatatu. Unatakiwa kuwepo shuleni tarehe hiyo. Toa taarifa mapema kama hutoripoti siku hiyo kabla hatua zingine hazijachukuliwa, mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2020.

2. TARATIBU NA HALI YA SHULE.
   Shule hii ni mchanganyiko (wavulana na wasichana) Wanafunzi wote wanapaswa kuwa makini kwa kuzingatia na kufuata taratibu zote za shule. Kupuuza na kukiuka taratibu za shule kwa makusudi kutasababisha wanafunzi kuachishwa masomo. Sheria za shule zimeambatanishwa. Hivyo zisome kwa makini na kuzielewa.

3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.
   Sare za shule na vifaa ambavyo mzazi anatakiwa kumwandalia mwanafunzi.
   (a) Sare ya shule:
   (i) Wavulana – Suruali jozi mbili (i) kitambaa cha kijani mgomba (ii) kitambaa cheusi, viwe ni vitambaa vya suti na ziwe na upana chini wa inchi kumi na sita (16) mzunguko, pia na suruali iwe na rinda 2 kila upande na mifuko 3, mbele miwili na nyuma mmoja. Shati nyeupe mikono mifupi jozi mbili (2), viatu vyeusi vya kufunika vyenye visigino vifupi na vyenye kufunga na kamba, Soksi nyeupe jozi mbili.
   (ii) Wasichana – Sketi jozi mbili(i) kitambaa cha kijani mgomba (ii) kitambaa cheusi, viwe ni vitambaa vya suti mashono rinda kumi na sita (16) urefu wa kutosha hadi chini mkanda wake (waist band) usizidi inchi mbili zitakaguliwa shuleni. Viatu vyeusi vya kufunika vyenye visigino vifupi na vyenye kufunga na kamba, Soksi nyeupe jozi mbili. Sample za vitambaa zinapatikana shuleni.
   (b) Rangi ya Hijabu – Rangi ya hijabu kitambaa cheupe kwa wasichana.
   (c) Sare ya Michezo.
      (i) T – Shirt rangi nyekundu yenye michirizi mweupe mkononi kwa wote (wavulana na wasichana)
      (ii) Viatu vya raba kwa wote wavulana na wasichana.
      (iii) Track suit ya rangi nyekundu kwa wasichana, na wavulana bukta rangi nyekundu.

<u>CHAKULA</u>: Mahindi kg.10, maharage, Choroko, Kunde, au Dengu kg.5, na Tshs. 3,000/= ya mpishi kwa miezi mitatu pamoja na matumizi mengine.

4. VIFAA VYA MASOMO.
   Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo siku ya kuripoti shuleni.
   (i) Madaftari makubwa (Counter book) kumi na tano (10)
   (ii) Mkebe wa vifaa vya hisabati.
   (iii) Dictionary ili imsaidie kujifunza kiingereza kwa urahisi (ni ya lazima)
   (iv) Mfuko wa kubebea daftari zake (School bag).
   (v) Mfagio 1 aina ya chelewa.
   (vi) Ndoo ndogo kwa ajili ya usafi. (vii) Passport size 1, (viii) Plastic file 1

FOMU YA MAMBO BINAFSI NA MIKATABA YA MWANAFUNZI/MZAZI/MLEZI NA SHULE (PERSONAL PARTICULARS)
(IJAZWE KWA HERUFI KUBWA)

1. Jina kamili ....
2. Tarehe ya kuzaliwa
   Tarehe; ....mwezi ....mwaka ....
3. Uraia: ....kabila: ....
4. (a) Anwani kamili ya nyumbani (yaani kwa wazazi)
   ....
   ....
   ....
   (b) Wakati wote wa masomo taja mahali utakapokaa ....
5. Jina la Mzazi/Mlezi ....hai/amefariki

   Anwani yake ....

   Eneo analoishi ....

   Simu: ....

<u>TAMKO LA MWANAFUNZI.</u>

6. (a) Mimi ....ninakiri na kukubali kwamba kipindi chote cha masomo sitajihusisha na migomo/fujo/makosa ya jinai ikitokea sheria zichukue mkondo wake.
   Jina ....sahihi ....tarehe ....

<u>TAMKO LA MZAZI/MLEZI.</u>

(b) Mimi ....Mzazi/Mlezi wa ....ninakiri na kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule, na pia nitatekeleza maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
Jina ....sahihi ....tarehe ....

7. (a) Majina ya ndugu wa kiume: 1. ....
   2. ....
   3. ....
   4. ....

   (b) Majina ya ndugu wa kike: 1. ....
   2. ....
   3. ....
   4. ....

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatavyo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.
2. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
3. Mahudhurio mazuri katika vipindi vya ndani na nje ya darasa ni muhimu.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kuvuta sigara, kufuga kucha ndefu, kufuga ndevu, kuvaa mavazi yasiyo na heshima, kupaka rangi ya kucha au midomo, kunyoa kipara, wala kupigana au kugombana, kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
5. Kuvaa sare ya shule wakati wote wa masomo darasani, kutoka nje ya shule kwa shughuli maalumu, kwenda hospitalini na maandamano.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.

1. Wizi.
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubel n.k.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

Naambatanisha na fomu zifuatazo.

(i) Medical Examination Form ambayo itatakiwa kujazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Pia fomu hii aje nayo mwanafunzi siku ya kuripoti shuleni.

(ii) Naambatanisha pia fomu ya historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa shuleni.

(iv) Siku ya kuripoti mwanafunzi aje shuleni na Mzazi au Mlezi.

(v) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

....

WILFRED J. OGEJO

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI SEN... MASWA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

SENG'WA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 367,
MASWA – SIMIYU.

FORM FOR MEDICAL EXAMIANTION.

Please examine the above mentioned He/She as to her/his fitness for studies in this school. (This form must be filled in by the government medical officer).

Student's full name: ....

Present age: ....

Blood test: ....

Stool examination: ....

T.S Test: ....

Asthma: ....

Eye disorder: ....

Norse disease: ....

Anaemia: ....

Chest: ....

Operations:...

Serious accidents: ....

Pregnancy: ....
(in case of female)

ADDITIONAL INFORMATION Eg. Physical defects or impairment, chronically family diseases etc.

....

I certify that I have personally examined He/She ....

And found him/her/fit/unfit to pursue further studies.

Signature ....Designation ....

Official Stamp ....Mobile No. ....